WIZARA YA NISHATI

NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 62 | Feb 1 - 28 2025



# UJENZI KITUO CHA KUPOZA UMEME HANDENI KUIMARISHA UPATIKANAJI UMEME- RAIS SAMIA

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Amanzi Kimonjo
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga

© NISHATI 2025

# UJENZI KITUO CHA KUPOZA UMEME HANDENI KUIMARISHA UPATIKANAJI UMEME- RAIS SAMIA

- Kituo kugharimu  shilingi bilioni 50
- Zaidi ya Shillingi billioni 98 kutekeleza mradi wa gridi imara Kilindi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Wilaya ya handeni mara baada  ya kuzindua Shule ya wasichana ya Kilindi na ofisi ya Halmashauri ya Wilaya hiyo katika ziara yake Mkoani Tanga.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema utekelezaji wa ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Handeni mkoani Tanga utakapokamilika utaboreha upatikanaji wa umeme katika Wilaya za Handeni  na Kilindi pamoja na maeneo jirani.

Rais Samia ameyasema hayo Februari 25, 2025 katika ziara yake mkoani Tanga wakati akizungumza na wananchi wa Handeni mara baada ya kuzindua Shule ya Wasichana ya Kilindi na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

"Tatizo la umeme hapa Handeni Serikali inalifahamu, imeanza kuchukua hatua kwa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kitakachogharimu takribani shilingi bilioni 50 za kitanzania ambacho kitaboresha upatikanaji wa umeme." Amesema Rais Samia

Ameeleza kuwa, upatikanaji wa umeme wa uhakika Handeni utasaidia ukuaji wa uchumi pamoja na kuyainua madini ya kinywe ambayo yanapatikana Wilaya ya Kilindi na yanahitaji umeme wa kutosha.

Awali, Mbunge wa Kilindi, Mhe. Omari Kigua aliishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi kwa kutoa zaidi ya shilingi bilioni 98 kwa ajili ya kutekeleza mradi ya gridi imara utakao husisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkata kupitia Handeni hadi Kilindi.

Mhe. Kigua ameeleza kuwa Wilaya ya Kilindi ina Vijiji 102 ambavyo vyote vimefikiwa na umeme na sasa kazi inayoendelea ni ya kufikisha umeme kwenye Vitongoji.

# DKT. BITEKO AIKARIBISHA DUNIA KUWEKEZA SEKTA YA NISHATI

- Dkt. Samia aleta Mapinduzi ya Nishati Afrika
- Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia yaendelea kujadiliwa kimataifa




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Nishati kutoka India, Sudan, Malawi, Rwanda, Nepal, Brazil. Mkutano huo umefanyika Februari 12, 2025 jijini New Delhi nchini India ikiwa ni sehemu Wiki ya Nishati India (Kulia ni Waziri wa Petroli na Gesi Asilia wa India, Mhe. Hardeep Singh)

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewakaribisha wawekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani kuwekeza katika sekta ya nishati nchini.

Akizungumza Februari 12, 2025 jijini New Delhi nchini India katika Mkutano wa Mawaziri wa Nishati kutoka India, Sudan, Malawi, Rwanda, Nepal, Brazili pamoja na wakurugenzi wa kampuni mbalimbali kutoka India Dkt. Biteko amesema Serikali imeweka mazingira wezeshi ili kuhakikisha kuwa Nishati Safi ya Kupikia inapatikana kwa urahisi na gharama nafuu.

Ambapo mwaka 2022 Serikali ilisisitiza matumizi ya nishati safi na kueleza athari za matumizi ya nishati isiyokuwa safi kwa kuanzisha mjadala wa kwanza ambao uliongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Dkt. Biteko ametaja fursa mbalimbali za biashara ya Nishati Safi ya Kupikia nchini Tanzania, kama vile ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji, kupokea, kuhifadhi na kusambaza nishati safi ya kupikia.

Fursa zingine ni vituo vya kupokea LPG, vifaa vya uhifadhi, miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam na maeneo jirani, usambazaji wa LNG wa kiwango kidogo, vifaa na mitungi ya gesi asilia.

" Hivyo basi, ningependa kuchukua fursa hii kuwataka wadau wote na wawekezaji katika sekta ya nishati kujiunga nasi katika malengo yetu makubwa lakini yanayoweza kufikiwa ya kupata umeme na Nishati Safi ya kupikia, kuongeza sehemu ya nishati mbadala katika mchanganyiko wa nishati na kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi ili kusaidia upatikaji wa nishati," amesema Dkt. Biteko.

Hata hivyo, ametaja jitihada za Serikali za kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia "Tanzania imekamilisha maendeleo ya Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa mwaka 2024-2034 wenye lengo kuu la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia Nishati Safi ya Kupikia ifikapo




Mawaziri wa Nishati kutoka India, Sudan, Malawi, Rwanda, Nepal, Brazil wakiwa kwenye Mkutano wa Mawaziri wa Nishati uliofanyika leo Februari 12, 2025 jijini New Delhi nchini India ikiwa ni sehemu Wiki ya Nishati India

mwaka 2034, "

Ameongeza " Katika kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi zingine tumegundua kuwa India imefanya vizuri kwani takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 2023, asilimia 71.1 ya watu wa India walikuwa wakitumia nishati safi ya kupikia. Hii imetokana na umuhimu wa kuhusisha sekta binafsi na kuunganishwa kwa ruzuku kwa kaya zenye kipato cha chini,"

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amesema " Kulingana na takwimu, takriban watu bilioni 2.3 duniani hawapati nishati safi ya kupikia na watu milioni 990 katika Sub-Sahara Afrika hawafikiwi na nishati safi. Hali hii inasababisha matatizo ya afya, uharibufu wa mazingira na matatizo ya kiuchumi,"

Vilevile, amesema Rais Samia amedhamiria kuipeleka ajenda ya nishati safi ya kupikia nje ya mipaka ya Tanzania na Afrika, ambapo katika mkutano wa COP 28, alizindua Programu ya Uwezeshaji wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Wanawake wa Afrika (AWCCSP), iliyoelekezwa kukabiliana na changamoto kubwa za kijinsia, mazingira, afya, na kiuchumi zinazowakabili wanawake na wasichana barani humo.

Akiendelea kuelezea msimamo wa Tanzania katika kuhamasisha Ajenda ya Matumizi ya Nishati Safi kimataifa, Dkt Biteko amesema mwaka 2024 Rais Samia alishiriki katika Mkutano wa Juu wa Nishati Safi ya Kupikia nchini Ufaransa ambapo alihudumu kama mwenyekiti mwenza na takriban dola bilioni 2.2 ziliahidiwa kwa ajili kusaidia ajenda hiyo barani Afrika.

Aidha, Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Nishati ya Afrika (AFREC) ilifanya Mkutano wa Kiwango cha Juu kuhusu Kupikia Nishati Safi barani Afrika katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mnamo Septemba 2024 pamoja na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliyofanyika jijini Dar es salaam Februari 27 na 28 mwaka huu kwa ajili ya kueleza dhamira zao juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Nishati ya Kitaifa.

Kwa upande wake, Waziri wa Petroli na Gesi Asilia wa India, Mhe. Hardeep Singh ametaja madhara ya matumizi ya nishati isiyosafi " Kumekuwepo na idadi ya vifo takribani milioni 2, lakini wanawake na watoto wanapata madhara zaidi, huku wanawake wakitumia hadi saa 5 kila siku kwa ajili ya kutafuta kuni na kuandaa chakula,"

Akielezea mafanikio ya matumizi ya nishati safi nchini India, amesema sasa watu milioni 330 wameunganishwa na matumizi ya nishati safi.

"Nishati safi sasa inapatikana kwa watu na maisha yamekuwa rahisi na shughuli zimeendelea kufanyika kwa ufanisi, sioni kwa nini hatuwezi kufanya hivi kwa kila mwananchi inawezekana." Amemalizia Mhe. Signh

Kimsingi mkutano huo wa Mawaziri wa Nishati unatajwa kuwa muhimu katika jitihada za kuendeleza matumizi ya nishati safi duniani ambao umetoa fursa kwa mawaziri waliohudhuria kueleza jitihada zinazofanyika za kukuza matumizi ya nishati safi katika nchi zao.

Aidha, kwa ujumla masuala ya sera, mila za watu, uhamasishaji, ubunifu, miundombinu ya usambazaji na wawekezaji yanatajwa kuwa na mchango muhimu wa mafanikio ya matumizi ya nishati safi.

# DKT. BITEKO AIKARIBISHA INDIA KUWEKEZA MIRADI YA UMEME JUA NCHINI

- Asema suala la Tanzania kuwa na nishati ya uhakika si la kusubiri
- Kampuni ya Kimataifa ya Umeme Jua (ISA) tayari imeonesha nia ya kuwekeza
- Kituo cha umahiri wa umeme jua kuzinduliwa Arusha Juni mwaka huu



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati) akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kimataifa ya Umeme Jua (ISA) kutoka nchini India, Bw.Ajay Mathur ambayo imeonesha nia ya kuwekeza kwenye miradi ya umeme jua Tanzania. Mazungumzo hayo yamefanyika jijini New Delhi nchini India.


Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kimataifa ya Umeme Jua (ISA), Bw. Ajay Mathur ya nchini India ambayo ameialika kuwekeza kwenye miradi ya umeme jua nchini.

Mazungumzo hayo kati ya Dkt. Biteko na Bw. Mathur yamefanyika jijini New Delhi nchini India ambapo pia Dkt. Biteko aliwasilisha mada katika mikutano mbalimbali ya Wiki ya Nishati India.

" Tunawaalika mje kuwekeza Tanzania kwani tunahitaji kuwa na miradi mingi ya umeme kutoka vyanzo tofauti ili kuweza kutosheleza mahitaji ya watu wetu na kinachotupa msukumo zaidi kwa sasa ni mpango mahsusi wa misheni 300 tuliousaini mwezi Januari 2025 ambapo Tanzania tunapaswa kupeleka umeme kwa wananchi milioni 8.3 ifikapo mwaka 2030." Amesema Biteko

Dkt. Biteko ameishukuru kampuni ya ISA kwa kuona Tanzania kama sehemu sahihi ya uwekezaji na kueleza kuwa kazi yake ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na miradi mingi ya nishati ambayo italeta utoshelevu wa umeme na kuchagiza maendeleo.

Kuhusu miradi ya umeme Jua nchini, Dkt. Biteko amesema Tanzania imeanza kutekeleza mradi wa umeme jua wa megawati 150 wilayani Kishapu mkoani Shinyanga kwa kuanza na megawati 50 ambapo megawati 100 zitaanza kutekelezwa baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kimataifa ya Umeme Jua (ISA) kutoka nchini India, Bw.Ajay Mathur (wa Pili kushoto) ambayo imeonesha nia ya kuwekeza kwenye miradi ya umeme jua Tanzania. Mazungumzo hayo yamefanyika jijini New Delhi nchini India. Wengine katika picha ni Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbega (wa kwanza kushoto) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa pili kulia).

Ameongeza kuwa, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pia limepata maeneo matatu kwa ajili ya miradi ya umeme jua ambayo ni Zuzu, Dodoma (MW 60), Mkwese, Manyoni - Singida (MW 199) na Same, Kilimanjaro (MW 50).

Ili kuwezesha uwekezaji wa kampuni hiyo nchini, Dkt. Biteko amewataka Watendaji hao kuainisha maeneo ambayo wanahitaji kuwekeza ili Wataalam waanze kuyafanyia kazi.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ISA, Ajay Mathur alimweleza Dkt.Biteko kuwa kampuni hiyo inataka kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya umeme jua nchini huku msukumo wakiupata pia kutoka kwenye Mkutano wa Misheni 300 ambao ulieleza nia ya Afrika kufikisha umeme kwa watu milioni 300 Tanzania ikiwemo.

Amesema kampuni ya ISA inafanya kazi kwenye nchi 120 duniani na inashirikiana na Serikali mbambali katika utekelezaji wa miradi ya umeme jua kwa njia mbalimbali ikiwemo kutoa mafunzo kwa wazawa kuhusu utengenezaji wa vifaa vya umeme jua, kusaidia serikali kutengeneza sera zinazowezesha uwekezaji katika nishati ya jua, kutoa maarifa kwa wahandisi wa nishati ya jua na watunga sera za nishati.


Katika hatua nyingine, Mathur amesema kuwa tayari kampuni ya ISA imeanza kufanya kazi Tanzania kwa kuwa na kituo cha Teknolojia ya Jua (STAR-C) ambacho kitakuwa na majukumu mbalimbali ikiwemo kuandaa mtaala na skimu za mafunzo sekta ya nishati ya jua na kuimarisha uwezo wa ndani wa kupima ubora wa vifaa vya jua kulingana na viwango vya kimataifa.

Vilevile kituo hicho kitasaidia ubunifu wa bidhaa na huduma zinazohimiza matumizi ya nishati ya jua, pamoja na kusaidia biashara katika mnyororo wa thamani wa sekta hiyo.
Ameongeza kuwa kituo hicho ambacho kimejengwa katika Chuo cha Ufundi Arusha kitazinduliwa mwezi Juni mwaka huu.
Kwa Afrika, ISA imeanzisha vituo vya STAR C nchini Ethiopia, Somalia, Ivory Coast na Ghana ambapo tangu kuanzishwa kwake vituo hivyo vimefundisha maelfu ya wataalamu katika sekta ya nishati ya jua.

Mazungumzo kati ya Dkt. Biteko na Bw.Mathur yalihudhuriwa na Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbega na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.

# PURA ENDELEENI KUWAVUTIA WAWEKEZAJI KATIKA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI - KAPINGA

- Ataka Duru ya Tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kuwa na matokeo chanya
- Aipongeza PURA kuwashirikisha Watumishi kujadili mipango ya Bajeti ya Taasisi



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga akizungumza na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) wakati wa Kikao cha Baraza hilo linalofanyika tarehe 18 na 19 Februari 2025, mkoani Morogoro.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga ameielekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) kuendelea kuvutia uwekezaji katika vitalu vilivyo wazi vya mafuta na gesi asilia ili kuongeza kiasi cha nishati hiyo nchini.

Mhe. Kapenga amesema hayo leo wilayani Morogoro, Mkoa wa Morogoro wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa PURA kinacholenga kujadili masuala mbalimbali ikiwemoMpango na Bajeti ya Taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/26.

“ Mkifanikiwa kuvutia uwekezaji katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi, nchi itaongeza ugunduzi wa rasilimali hiyo muhimu ikiwa ni pamoja na kuogeza futi za ujazo wa gesi inayopatikana nchini, Pia mkiendelea kuvutia uwekezaji kupitia Duru ya Tano ya kunadi vitalu itakayozinduliwa mwezi machi mwaka huu, pamoja na faida zilizopo, mtakuwa mmeendeleza jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuendelea kuifungua Tanzania kiuchumi na kuvutia uwekezaji zaidi.”Amesema Kapinga

Amesema Wizara ya Nishati inatambua umuhimu wa tukio la Duru ya Tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini pamoja na kutambua kazi kubwa ambayo imeshafanyika kuelekea uzinduzi wa tukio hilo ambalo amesema kuwa ni



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga akiteta jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) Mhandisi. Charles Sangweni (kushoto). Kulia ni Katibu wa Baraza Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ( PURA) Ebeneza Mollel,wakati wa Kikao cha Baraza hilo cha kujadili Mpango na Bajeti hilo linalofanyika tarehe 18 na 19 Februari 2025, mkoani Morogoro.

muhimu katika kuvutia uwekezaji zaidi katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

“ Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukizungumzia ugunduzi wa futi za ujazo trilioni 57.54 pekee ni wakati sasa wa kufanya zaidi na zaidi ili tuweze kuongeza ugunduzi wa rasilimali hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa.” Amesisitiza Mhe.Kapinga

Katika kikao hicho cha Baraza la Wafanyakazi, ameupongeza uongozi wa PURA kwa kuendelea kuwashirikisha watumishi wake katika kujadili, kupanga na kupitisha mipango na Bajeti ya Taasisi kwenye Baraza la Wafanyakazi ikiwa ni utekelezaji pia wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma.

Amesema kufanyika kwa vikao hivyo ni ishara tosha ya utawala bora mahala pa kazi kwa kuwa watumishi wanapata fursa ya kuchangia mawazo yao kuhusu hali ya uendeshaji wa Taasisi hivyo kuendelea kuwa ni sehemu muhimu ya Taasisi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) Mhandisi. Charles Sangweni, amesema duru ya tano (5) ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini inatarajiwa kuzinduliwa mwezi Machi, 2025 Jijini Dares salaam wakati wa Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki (EAPCE’25).

Amesema PURA inaendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu mbalimbali nchini na Kuhakikisha watanzania wazawa wanashirikishwa katika miradi mbalimbali ya mkondo wa juu wa petroli nchini.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) wakati wa Kikao cha Baraza hilo linalofanyika tarehe 18 na 19 Februari 2025, mkoani Morogoro. Kushoto Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) Mhandisi. Charles Sangweni.

# SERIKALI YAJIDHATITI KUBORESHA SEKTA YA KILIMO – DKT BITEKO

- Anadi soko la mazao jamii ya mikunde India
- Mnada mazao ya kunde mtandaoni waboresha biashara ya kimataifa
- Biashara kati ya Tanzania na India kufikia dola bilioni 7.9



aibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia katika Mkutano sekta ya Kilimo kwenye masuala ya mazao jamii ya mikunde. Mkutano huo umefanyika Februari 13, 2025 jijini New Delhi nchini India.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Serikali ya Tanzania imejidhatiti kuboresha na kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuja na mipango kadhaa yenye lengo la kuongeza fursa kwa wakulima nchini.

Dkt. Biteko amesema hayo Februari 13, 2024 jijini New Delhi, India wakati akishiriki mkutano kuhusu masuala ya mazao jamii ya mikunde.

"Tunaongeza uwekezaji katika utafiti na kuboresha upatikanaji wa teknolojia za kisasa za kilimo ambapo kila afisa wa ugani nchini amepewa vifaa vyote muhimu ikiwemo pikipiki na kompyuta ili kutoa huduma nzuri na kwa wakati kwa wakulima wetu." Amesema Dkt. Biteko

Amesema Serikali pia imeboresha shughuli za usafirishaji wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kurahisisha michakato ya uuzaji mazao "Tanzania inaendeleza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo itaimarisha usafirishaji wa bidhaa yenye urefu wa takribani kilomita 500 kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Dodoma ambayo imekamilika na na inatumika.

Vilevile, amesema kupitia mradi wa BBT (Building a Better Tomorrow) Serikali imewezesha vijana kwa kuwapa ardhi, fedha na upatikanaji wa masoko sambamba na kuongeza huduma za kifedha za kidijitali.

Aidha, Dkt. Biteko amesema "India ni soko muhimu kwa mazao jamii ya kunde kutoka Tanzania na tunaweza kupata mafanikio makubwa zaidi. Leo nawaalika wawekezaji kutoka India na nchi nyingine duniani kuja kuwekeza katika sekta ya kilimo ya Tanzania



Sehemu ya wawekezaji na wadau wa Kilimo waliojitokeza kwenye Mkutano sekta ya Kilimo kwenye masuala ya mazao jamii ya mikunde. Mkutano huo umefanyika Februari 13, 2025 jijini New Delhi nchini India.

kuanzia uzalishaji wa kisasa wa soya hadi uwekezaji katika mifumo ya usimamizi wa mavuno,"

Akizungumzia maendeleo ya sekta mazao jamii ya mikunde, amesema kuwa mwaka 2023, Tanzania ilizalisha takriban tani 250,000 za mbaazi, ikiwa ni ongezeko la asilimia 56 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Inakadiriwa ifikapo mwaka 2030 Tanzania itakuwa na ukuaji mkubwa katika Pato la Taifa kupitia Kilimo, ambapo mauzo ya maharage mekundu, mbaazi na choroko yanatarajiwa kufikia dola bilioni 1.47, dola milioni 84 na dola milioni 115. Aidha, ili kufikia uwezo huo, Tanzania imeweka mikakati ya kukuza sekta ya mazao jamii ya kunde kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa wakulima kusajiliwa, kuboresha mbinu za kilimo na teknolojia, kuhakikisha ubora na viwango vya mazao kulingana na mahitaji ya soko.

Pamoja na hayo Dkt. Biteko amesema "Mazao jamii ya kunde



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea zawadi ya maua kutoka kwa Mwenyekiti wa India Pulses and Grains Association (IPGA), Bimar Kothar wakati wa Mkutano wa mazao jamii ya mikunde uliofanyika Februari 13, 2025 jijini New Delhi nchini India




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwa kwenye picha ya pamoja na Balozi wa Tanzania nchini India Mhe. Anisa Mbega na Viongozi wa Wizara ya Kilimo alipotembelea Banda la Wizara ya Kilimo likiongozwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde kwenye mkutano wa mazao ya jamii ya mikunde uliofanyika Februari 13, 2025 jijini New Delhi nchini India

nchini Tanzania yanauzwa kupitia mnada wa mtandaoni ambao unatoa fursa kwa wafanyabiashara kupata taarifa kuhusu mizigo iliyohifadhiwa katika ghala lililosajiliwa,"

Amesisitiza "Mfumo huu unahakikisha uwazi, ufuatiliaji na ufanisi katika biashara ya kimataifa. Mwaka 2024 pekee kupitia mfumo huu, wakulima wa Tanzania walipata zaidi ya dola milioni 91.31 kutoka katika biashara ya mbaazi, dengu na maharagwe ya soya, ubunifu huu si tu unaimarisha ushindani wetu bali pia unafungua fursa mpya za ushirikiano,"

Kufuatia hali hiyo, kiwango cha biashara kati ya nchi hizo mbili kimeongezeka na kufikia dola bilioni 7.9 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia, mwaka 2023 mauzo ya mbaazi kutoka Tanzania kwenda India yalifikia tani 186,447 yenye thamani ya dola milioni 139.1




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (wa pili kushoto) akifuatilia Mkutano wa mazao jamii ya mikunde uliofanyika Februari 13, 2025. Wa kwanza kushoto ni Waziri wa Masoko na Itifaki Serikali ya Maharasta, Mhe. Jaykumar Rawal, wa tatu kushoto ni Waziri wa watuamiaji Chakula na Usambazaji wa Umma na Waziri wa Nishati Mpya na Jadidifu, Mhe. Pralhad Joshi

# TANZANIA YATUMIA WIKI YA NISHATI INDIA KUNADI VITALU VYA MAFUTA NA GESI ASILIA NCHINI

- Lengo ni kuvutia uwekezaji katika Mafuta na Gesi Asilia Bahari kuu na Nchi kavu
- Dkt. Biteko aipongeza PURA kutumia majukwaa Kimataifa kutafuta wawekezaji
- Atilia mkazo uendelezaji wa vyanzo vyote vya nishati
- Vitalu 26 vya Mafuta na Gesi Asilia kunadiwa




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (wa pili kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mhandisi Carles Sangweni (wa tatu kushoto) akieleza kuhusu PURA inavyohamasisha wawekezaji mbalimbali duniani kushiriki katika Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Bahari Kuu ya Hindi na Nchi Kavu kupitia Kongamano na Maonesho ya Wiki ya Nishati ya India yanayofanyika katika Jiji la New Delhi, India.

Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli Tanzania (PURA) imeendelea kuhamasisha wawekezaji mbalimbali duniani kushiriki katika Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Bahari Kuu ya Hindi na Nchi Kavu itakayozinduliwa mwezi Machi mwaka huu.

Matangazo ya fursa za uwekezaji kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia yanaendelea kupitia Kongamano na Maonesho ya Wiki ya Nishati ya India yanayofanyika katika Jiji la New Delhi, India tukio ambalo linawashirikisha zaidi ya watu 70,000 kutoka nchi zaidi ya 50 Duniani.

Katika Banda la Tanzania kwenye Maonesho hayo washiriki wengi wamevutiwa na taarifa za kijiofizikia zinazobainisha utajiri wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia zilizopo Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ambaye anashiriki Kongamano hilo, ametembelea banda hilo la Tanzania na kuipongeza PURA kwa kutumia majukwaa ya kitaifa na kimataifa kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, lengo la Serikali ni kuhakikisha vyanzo vyake vyote vya nishati vinaendelezwa ili kuwa na uhakika wa nishati ya kutosha wakati wote. Katika kuelekea kwenye duru hiyo ya Tano ya Kunadi Vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni amesema PURA imekamilisha masuala mbalimbali ikiwemo kupata Kampuni ya Kijiofizikia iitwayo TGS ASA yenye utaalam wa kuchakata data za mafuta na gesi asilia ambayo pia inahusika na utangazaji wa data hizo katika masoko mbalimbali duniani .



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika banda la Wizara ya Umeme nchini India ili kufahamu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara hiyo katika Kongamano na Maonesho ya Wiki ya Nishati ya India yanayofanyika katika Jiji la New Delhi, India. Kushoto kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ni Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe.Anisa Mbega.

Mhandisi Sangweni amesema kampuni hiyo itatakiwa kukusanya na kuchakata data za mitetemo katika maeneo mengine ya bahari kuu ambayo hayajafanyiwa kazi ili kuongeza taarifa na data za petroli kwa wawekezaji.

Ameongeza kuwa, PURA imeshakamilisha uandaaji wa ramani inayoonesha maeneo ambayo yatatangazwa kwenye duru ya tano inayojumuisha vitalu 26 ambapo vitalu 23 viko kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi na vitalu vitatu vipo Ziwa Tanganyika.
Amesema Duru ya tano ya Kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia itafanyika mwezi Machi, 2025 katika Mkutano na Maonesho ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Petroleum Conference and Exhibitions (EAPCE'25) Jijini Dar es Salaam.

Maonesho hayo yatakwenda pamoja na maonesho ya kitaalam kuhusu jiolojia ya mafuta na gesi asilia ya Tanzania; wawekezaji kuangalia taarifa za kijiolojia, kununua zabuni, kuwasilisha zabuni, kufanya tathmini ya zabuni zilizowasilishwa na kupokelewa, kufanyika kwa majadiliano ya mikataba (PSAs), kupata idhini ya Serikali ya kusaini PSAs kutoka Wizara ya Nishati na Baraza la Mawaziri na Kusaini Mikataba kati ya Serikali na Wawekezaji wawatakaoshinda

Ametaja faida mbalimbali zitakazopatikana baada ya Serikali kunadi vitalu hivyo kuwa ni kuongezeka kwa mapato ya kodi kwa Serikali, mirabaha na gawio la faida itokanayo na rasilimali itakayogundulika, mauzo ya data na tozo za leseni pamoja na kutoa fursa ya ajira kwa Watanzania na kazi kwa makampuni ya kitanzania,.
katika Kongamano hilo linaloendelea nchini India, Dkt. Biteko alipata fursa ya kutembelea na kuzungumza na Watendaji wa Wizara ya Umeme ya India pamoja na Watendaji wa kampuni ya Shell ambayo ni moja ya wawekezaji katika mradi wa LNG ambapo aliwaeleza Watendaji wa Shell kuwa Serikali inataka kuona majadiliano yanakamilika na mradi unaanza kutekelezwa.

Dkt. Biteko alifuatana na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambao ni Mhe. Juliana Masaburi, Mhe. Ussi Pondeza na Mhe. Iddi Kassim Iddi.

# DKT. BITEKO ATETA NA JUMUIYA YA WASAMBAZAJI WA MITUNGI YA GESI NCHINI

- Awashukuru kwa mchango wao utekelezaji Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia
- Ataka LPG ipatikane kwa wingi hadi ngazi ya Vijiji
- Ahimiza Tanzania kuwa kitovu cha usambazaji LPG Afrika Mashariki
- Tanzania yaendelea kupigiwa mfano Kimataifa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati wa kikao chake na Jumuiya ya Kampuni zinazohusika na Usambazaji wa Mitungi ya Gesi (LPG) -TZLPGA kwa lengo la kuwashukuru kwa mchango wao katika utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia pamoja na kujadiliana masuala mbalimbali ikiwemo utatuzi wa changamoto zinazoikumba TZLPGA ili kuhakikisha wanatoa huduma kwa urahisi nchi nzima. Mazungumzo yamefanyika leo jijini Dodoma

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Jumuiya ya Kampuni zinazohusika na Usambazaji wa Mitungi ya Gesi (LPG) -TZLPGA kwa lengo la kuwashukuru kwa mchango wao katika utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia pamoja na kujadiliana masuala mbalimbali ikiwemo utatuzi wa changamoto zinazoikumba TZLPGA ili kuhakikisha wanatoa huduma kwa urahisi nchi nzima.

Mazungumzo kati ya Dkt. Biteko na Jumuiya hiyo yamefanyika leo Februari 20, 2025 jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba pamoja Watendaji kutoka.Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ( EWURA) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini ( REA).

"Ili Serikali ifanikiwe lazima kuwashirikisha watu wake, tunawashukuru sana kwa mchango wenu katika kufanikisha Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia ambao kutoka tuuzindue mwaka 2024, uelewa na matumizi ya mitungi ya gesi umeendelea kuongezeka, mitungi hii ni gharama lakini ninyi mnajitoa na kutuunga mkono." Amesema.Dkt.Biteko

Hata hivyo Dkt.Biteko amezitaka kampuni hizo kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa mitungi ya gesi inafika kwa wingi hadi ngazi ya vijiji ili kuweza kufikia lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya wananchi wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2030 ikiwa pia ni utekelezaji wa Mpango wa Mahsusi wa Nishati ( Energy Compact uliosainiwa mwezi Januari 2025.

Amesema kuwa lengo la kikao hicho pia lilikuwa ni kujadili changamoto ambazo kampuni hizo wanakutana nazo ikiwemo za kikodi ambazo zina nafasi ya kujadiliwa katika Muswada wa Masuala ya Fedha utakaosomwa katika Bunge la Bajeti la mwaka 2025/2026.

"Tumekutana hapa ili tunapoelekea kwenye Bajeti ya Serikali mtuambie kipi tukiboreshe kupitia Muswada wa Masuala Fedha na ni vizuri pia mkatueleza jambo gani lifanyike ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi." Ameeleza Dkt. Biteko

Kuhusu Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia amesema kuwa, "Tangu tulipozindua Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia tumepata ushirikiano mkubwa sana Afrika na duniani kote kupitia diplomasia ya Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na tumeendelea kupata fursa kubwa ya kuonesha na kuuelezea Mkakati



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (kulia) akizungumza wakati wa kikao chake na Jumuiya ya Kampuni zinazohusika na Usambazaji wa Mitungi ya Gesi (LPG) -TZLPGA

wetu, pia tunaalikwa na nchi mbalimbali hata ambazo zimepiga hatua kuliko sisi, hii inaonesha kwa vitendo dhamira yetu ya kuhakikisha watu wanahama kutoka kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kwenda kwenye nishati safi ya kupikia." Amebainisha Dkt. Biteko

Amesema mwaka 2021 idadi ya watumiaji wa Nishati Safi ya Kupikia nchini ilikuwa asilimia 9 pekee. Aidha, wakati Mkakati huo unazinduliwa Mei 2024 hadi Februari 2025 watumiaji wamefikia asilimia 33 hivyo ni hatua nzuri katika kufikia lengo la Serikali la kufikisha asimilia 80 ya watumiaji wa Nishati Safi ya Kupikia ifikapo mwaka 2034.

Ameeleza kuwa changamoto inayoikabili Serikali katika kuhamasisha wananchi kutumia Nishati Safi ya Kupikia ni uwepo wa nishati mbadala ambazo si safi za kuni na mikaa ukilinganisha na nchi zingine ambazo hazina urahisi wa upatikanaji wa kuni na mkaa, hivyo ametaja mbinu ya kukabiliana na changamoto hiyo kuwa ni kuendelea kutoa elimu mara kwa mara ili kusaidia wananchi kubadili tabia na mitazamo juu ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Akijibu baadhi ya hoja za wajumbe wa Jumuiya hiyo, hususan kuhusu ombi la unafuu wa kodi katika bidhaa za gesi, amesema suala hilo limepokelewa na litafanyiwa kazi na Serikali.

Vilevile, ameishauri Jumuiya hiyo kutumia vyombo vya habari kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya Kulipia.

Aidha, ametoa changamoto kwa Jumuiya hiyo kutumia fursa ya Bandari kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usambazaji wa mitungi ya gesi katika Ukanda wa Afrika Mashariki ambayo ni faida ya kichumi kwa nchi na pia kuwezesha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felschemi Mramba amesema kuwa Serikali inaendelea na mikakati ya kuwa hifadhi maalum za mafuta ambapo suala la hifadhi maalum ya mitungi ya gesi linaangaliwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kampuni zinazohusika na Usambazaji wa Mitungi ya Gesi (LPG) nchini ( TZLPGA), Hamisi Ramadhani amemshukuru Dkt. Biteko kwa kuitisha kikao na Jumuiya hiyo ili kujadili masuala ya kiutendaji ambayo yanalenga kuhakikisha kampuni hizo zinaendelea kufanya biashara kikamilifu na gesi ya mitungi inapatikana katka maeneo yote nchini kwa wakati wote.

Ramadhani amesema kuwa, kampuni zinazohusika na usambazaji wa mitungi ya gesi zinapata ushirikiano mzuri kutoka Serikalini kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ( EWURA) kwa kutengeneza sheria zinazoongoza biashara ya LPG, Wakala wa Nishati Vijjini ( REA) kwa kutekeleza programu mbalimbali za Nishati Safi ya Kupikia na Shirika la Viwango Tanzania ( TBS) kwa kuweka viwango (standards) zinazoongoza biashara ya LPG.

Ameipongeza EWURA pia kwa kuwa mdhibiti bora kwani mara zote imekuwa ikisikiliza maoni ya wadau na kuyafanyia kazi kwa maslahi ya pande zote mbili ambazo ni Serikali na Wafanyabiashara.

Ameongeza kuwa mitungi ya gesi imesambaa sana sehemu za mijini kuliko vijijini hata hivyo kampuni hizo zinajitahidi ili biashara hiyo iendelee kushamiri maeneo ya vijijini pia ikiwa ni jitihada za kuhakikisha asilimia 75 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2030.

Katika hatua nyingine, Jumuiya hiyo imesema ipo tayari kushirikiana na Serikali ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usambazaji wa LPG katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki.

# DKT. BITEKO AITAKA EWURA KUFANYA KAZI BILA KUYUMBISHWA, KUPINDISHWA

- Vibali vituo vipya CNG vyatolewa, gharama za leseni zapunguzwa
- Morogoro, Makambako, Mbeya kutumika kushusha mafuta kutumia bomba la mafuta
- Afungua Baraza la Wafanyakazi EWURA
- Asisitiza mazingira mazuri, mafunzo kwa Watumishi




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati) akiwa ameshikana mikono kuashiria umoja kwa wafanyakazi wakati wa kufungua kikao cha nne cha Baraza la Pili la EWURA leo Februari 17, 2025 jijini Tanga. Kutoka kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. James Mataragio, Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian. Kutoka kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga Mhe. Japhari Kubecha na Mkurugenzi Mkuu EWURA Dkt. James Andelile

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameuagiza uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuhakikisha kunakuwa na uendelevu wa upatikanaji wa mafuta kwa wakati wote kwa gharama halisi, kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya sheria na kutatua malalamiko ya wateja kwa haraka ili kuendelea kutoa huduma bora kwa Watanzania.

"Nawahakikishia kuwa wakati wote Serikali itaendelea kuwapa kila aina ya ushirikiano ili muweze kuwahudumia Watanzania, Serikali yoyote inapata heshima ikiwa inawahudumia wananchi ambao wana umeme na mafuta wakati wote hivyo, fanyeni kazi kwa kufuata sheria ili muwe salama, msikubali kuingiliwa na kupindisha misingi ya kazi."Amesema Dkt. Biteko

Amesema hayo leo Februari 17, 2025 jijini Tanga wakati akifungua Kikao cha Nne cha Baraza la Pili la EWURA.

Dkt. Biteko ameipongeza EWURA kwa kutekeleza maagizo yake aliyoyatoa wakati wa kikao cha Baraza kilichofanyika mwezi Novemba 2024 ikiwemo kuongeza kasi ya kushughulikia malalamiko ya wateja, kuondoa urasimu katika utoaji wa vibali vya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi kwenye magari ( CNG), kupunguza gharama ujenzi wa vituo vya CNG, kulegeza masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini na kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Kutokana na maagizo hayo ya Dkt. Biteko, kati ya Novemba 2024 na Januari 2025 EWURA imetoa vibali vya ujenzi wa vituo vinane vya CNG huku wawekezaji 50 wakionesha nia ya kujenga vituo vingine.

Aidha, EWURA imeshusha gharama za leseni na vibali vya ujenzi vituo vya CNG na




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na wajumbe wa Baraza la Pili la EWURA wakati wa kufungua kikao cha nne cha Baraza hilo leo Februari 17, 2025 jijini Tanga

gharama za maombi ya vibali zimepunguzwa kutoka shilingi 500,000 hadi 50,000 na gharama za maombi ya leseni zimeshushwa kutoka 1,000,000 hadi 100,000.

Dkt. Biteko pia ametoa maagizo mbalimbali kwa uongozi wa EWURA ikiwemo kusimamia malipo na stahiki zote za kifedha za watumishi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwa na vifaa na vitendea kazi vya kisasa vinavyoendana na muda, teknolojia na mahitaji yaliyopo kwa Taasisi na watumishi.

Maagizo mengine aliyoyatoa ni kuwaendeleza watumishi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, mfupi na wa kati katika fani mbalimbali ili kuisaidia Taasisi na watumishi kuendana na mabadiliko na maendeleo ya Teknolojia yanayotokea ulimwenguni. Pamoja na kuboresha uhusiano kati ya uongozi na watumishi kwa kuanzisha mijadala ya wazi kuhusu maendelo na mipango ya baadaye ya Taasisi.

" Pia ni muhimu kutambua na kuthamini kazi nzuri za watumishi, vitu kama vyeti, barua za pongezi na tuzo za ufanisi husaidia kuwafanya watumishi watambue kwamba wanathaminiwa na hivyo kuendelea kuongeza bidii." Amesema Dkt. Biteko

Vilevile, amesisitiza suala la motisha kwa wafanyakazi na kuanzisha utamaduni wa kufanya mazoezi na kushiriki michezo ndani ya taasisi na kwa kushirikiana na Taasisi nyingine.

Katika kikao hicho ambacho kitajadili bajeti ijayo ya mwaka 2025/26 na utekelezaji wa bajeti ya 2024/2025, Dkt. Biteko amewahimiza wajumbe kujadili utekelezaji wa malengo ya taasisi kwa kuzingatia ajenda ya Taifa katika masuala ya Nishati hususani matumizi ya nishati safi ya kupikia na upatikanaji wa maji kwa gharama inayostahili kwa wananchi wote.

"Naamini mtafanya tathmini kutoka katika Bajeti iliyopita na kuona ni nini tufanye ili kukidhi mahitaji ya Watanzania." Amesema Dkt. Biteko.

Katika hatua nyingine Dkt. Biteko amesema kuwa, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipatia nchi heshima kubwa kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha kwa ajili ya kufadhili miradi hiyo.

Ameendelea " EWURA mnatakiwa kubeba ajenda hii ya nishati safi kwa kuelimisha umma kuhusu manufaa yake, pamoja na nishati safi ya kupikia tunataka kuongeza bomba la kusafirisha mafuta na kuongeza matenki ya kushusha mafuta maeneo mbalimbali ikiwemo Morogoro na Makambako ili tuweze kuondoa changamoto ya magari yote kuja kujaza mafuta Dar es Salaam."

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dkt. Batilda Buriani amesema kuwa EWURA imeendelea kusimamia ipasavyo mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa kuhakikisha kunakuwa na ushiriki kamilifu wa wazawa na maslahi mengine ya nchi.

Ameipongeza Ewura kwa kusimamia mwenendo mzima wa upatikanaji wa mafuta na hivyo kuwezesha mkoa huo kuwa na nishati ya mafuta ya kutosha.

Kuhusu umeme vijijini, amesema kuwa vijiji vyote 763 mkoani Tanga vina umeme huku kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 4,596 ikiendelea.

Akizungumzia utekelezaji wa Nishati Safi ya Kupikia, Dkt. Buriani amesema Mkoa wa Tanga unaendelea na uhamasishaji wa matumizi ya nishati hiyo, ambapo taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 zipatazo 1493 zipo kwenye mchakato wa kuhama kutoka kwenye matumizi ya kuni kwenda kwenye gesi huku Jeshi la Magereza likifanya vizuri zaidi kwa Magereza yake kuanza kutumia nishati safi.

Amesema mpaka sasa Tanga tayari imepokea mitungj ya gesi ipatayo 21,000 ambayo itatolewa kwa wananchi kwa bei ya ruzuku kwa punguzo la asilimia 50 na kwamba mitungi hiyo itaendelea kutolewa kadri inavyopatikana lengo likiwa ni kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio ameipongeza EWURA kwa kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko ikiwemo la kuhakikisha kunakuwa na vituo vingi vya kujazia gesi kwenye magari (CNG) ambapo kuanzia mwezi Novemba hadi sasa tayari wametoa vibali nane vya ujenzi wa vituo vipya vya CNG huku wawekezaji wakiendelea kujitokeza.

Aidha, ameipongeza EWURA kwa kuhamasisha suala la Nishati Safi ya Kupikia kwa kutoa elimu kwa wananchi na pia kuwezesha baadhi ya makundi ya wananchi kwa mitungi ya gesi ikiwemo vituo vinavyotoa malezi kwa wazee na shule.

Ameongeza kuwa, Ewura pia imefanya kazi kubwa kwenye usimamizi wa mradi wa EACOP kwa kuhakikisha maslahi ya nchi yanazingatiwa pamoja na ushiriki wa wazawa ambapo amesema mradi huo umefikia asilimia 55.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt.James Andilile alisema Taasisi hiyo imetekeleza ipasavyo maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Dkt.Biteko k wakati wa kikao cha Baraza hilo mwezi Novemba 2024 ikiwemo la kushughulikia kwa haraka malalamiko ya wateja yanayowasilishwa EWURA ambapo amesema kuwa kwa kupitia Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Ewura inashughulia malalamiko kwa haraka.

Kuhusu agizo alilolitoa Dkt. Biteko la EWURA kuhamasisha uwekezaji kwenye vituo vya kujazia gesi kwenye magari ( CNG) ili kuweza kuwa na vituo vingi, amesema agizo hilo limeendelea kutekelezwa ambapo kati ya mwezi Novemba 2024 na Januari 2025 tayari EWURA imetoa vibali vya ujenzi wa vituo 8 huku wawekezaji 50 wakionesha nia ya kuwekeza.

Dkt. Andilile amesema Ewura inaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini kwa kushirikiana na REA na kwa vituo vya CNG Ewura imelegeza masharti ya uwekezaji wa vituo ambapo maombi ya vibali yamepunguzwa gharama kutoka shilingi 500,000 hadi 50,000 na maombi ya leseni yamepunguzwa kutoka 1,000,000 hadi 100,000.

Aidha, kuhusu agizo alilotoa Dkt. Biteko kwa Ewura la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya Kupikia, Dkt. Andilile amesema kuwa taasisi hiyo imeendelea kutoa elimu kwa umma ikiwemo ya kuwaambia wananchi kuwa kuwa Gesi ya kupikia ni Salama.

Akizungumzia bajeti ya mwaka 2025/2026 itakayojadiliwa kwenye mkutano huo, Dkt.Andilile amesema kuwa Ewura imepanga kuwa na mifumo ya teknolojia itakayorahisisha kazi za udhibiti ili zifanyike kisasa na kwa ufanisi

# UTENDAJI KAZI KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA TANESCO WAMKWAZA DKT. BITEKO

- Amuagiza Mkurugenzi Mtendaji TANESCO kumchukulia hatua mtaalam aliyemfokea mteja
- Ataka Mpango Mahsusi wa Nishati uliosainiwa katika Mkutano wa Mission 300 kupewa kipaumbele
- PURA, REA, EWURA zang'ara tathmini ya utendaji kazi Taasisi chini ya Wizara ya Nishati



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati wa Kikao cha Tatu cha Tathmini ya Utendaji Kazi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati katika kipindi cha Oktoba-Desemba 2024 ikiwa ni utaratibu aliouanzisha kwa lengo la kujipima katika kila baada ya miezi mitatu ili kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara na Taasisi zake.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameeleza kutoridhishwa kwake na Kituo cha Huduma kwa wateja cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kusema huduma duni zinasababisha malalamiko kutoka kwa wateja.

Dkt. Biteko amesema hayo wakati wa Kikao cha Tatu cha Tathmini ya Utendaji Kazi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati katika kipindi cha Oktoba-Desemba 2024 ikiwa ni utaratibu aliouanzisha kwa lengo la wa kujipima katika kila baada ya miezi mitatu ili kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara na Taasisi zake.

"Pamoja na kazi zote nzuri mnazozifanya lakini eneo ambalo bado hatujafanya vizuri ni utoaji wa huduma kwa wateja, juzi nilitembelea kituo hiki nikawaambia sifurahishwi na utendaji kazi wa kituo, mimi nafahamu changamoto za kituo hiki si kwa kuota bali wananchi wananipa mrejesho pamoja na viongozi wanaonisimamia, hivi tumefanya kazi yote hii ya kuwa na umeme wa ziada, tunajenga laini za umeme, lakini mtu mmoja ambaye kazi yake ni kumsikiliza mteja na kumpa majibu sahihi anatupaint wote vibaya tunaonekana hatufai, majibu yapo lakini wataalam wanageuka kuwa wababe kwa wateja, hii hakubaliki." Amesema Dkt. Biteko

Dkt. Biteko ametolea mfano lalamiko la mwananchi la kupiga simu TANESCO kisha akapewa tiketi namba ya lalamiko lakini baada ya muda tiketi namba hiyo ilifutwa kwa madai kwamba lalamiko husika

limeshashughulikiwa huku ikiwa sikweli, hata hivyo baada ya mteja kuuliza kwa nini lalamiko lake limefutwa aliishia kufokewa.

Kutokana na hilo, Dkt.Biteko amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kuchukua hatua kwa mtaalam aliyehusika na suala hilo na endapo TANESCO haitachukua hatua ifikapo ijumaa wiki hii, atachukua hatua huku akisisitiza kwamba heshima kwa wananchi lazima iwepo na Wataalam wa Kituo cha Huduma kwa wateja wanapaswa kuwapa majibu stahiki na ya staha wananchi na wawe ni sehemu ya kutatua shida za wananchi.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameziagiza Taasisi zote chini ya Wizara ya Nishati kuupa kipaumbele Mpango wa Mahsusi wa Nishati (Energy Compact) ambao ulisainiwa katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika tarehe 28 Januari 20225 ambao pamoja na masuala mengine ya nishati, umelenga kusambaza umeme kwa watanzania milioni 8.3 ifikapo 2030.

“Kila mmoja kwa nafasi yake ajipange atatekeleza vipi hii Energy Compact, fedha hizi mlizosikia zimetolewa na wadau wa maendeleo kama Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika zinahusu Bara lote la Afrika, hazitakuja Tanzania pekee hivyo lazima tujipange jinsi ya kupata hizi fedha ili kutekeleza miradi tuliyopanga kuifanya na tumheshimishe Rais, Dkt. Samia kwa kushika nafasi ya kwanza katika utekelezaji Mpango huu mahsusi ambao ni muhimu katika Sekta yetu ya Nishati.” Amesema Dkt. Biteko

Aidha, ameuagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuhakikisha kwamba kazi ya usambazaji wa nishati safi ya kupikia vijijini inaenda sambamba na tathmini ya idadi ya watu wanaohama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda kwenye nishati safi na Taasisi ijipange kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 asilimia 75 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia.

Katika Kikao hicho cha Tathmini, Dkt. Biteko pamoja na Wizara ya Nishati walitoa zawadi kwa Taasisi zilizoshika nafasi za juu katika utendaji kazi ambazo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) iliyoshika nafasi ya kwanza, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ulioshika nafasi ya Pili na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ulioshika nafasi ya Tatu.

Pia ametoa zawadi kwa mikoa ya Kitanesco iliyofanya vizuri katika utendaji kazi ambayo ni Kilimanjaro (I), Kinondoni Kusini (II) na Kinondoni Kaskazini (III).

Kwa upande wake,, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga ameeleza kuwa vikao vya tathmini ya utendaji kazi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake ambavyo muasisi wake ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati vimeleta matokeo chanya kwa kuleta mabadiliko ya utendaji kazi kwa Wizara na Taasisi zake.

Amepongeza Watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi kubwa inayofanyika na inayoonekana katika macho ya wananchi ikiwemo uwepo wa nishati.

Mhe. Kapinga amewaasa watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kufanya kazi kwa umoja na kwa kujitoa ili kuendelea kumheshimisha Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Sekta ya Nishati kwa ujumla.

Taasisi zilizoshiriki Kikao cha Tatu cha Tathmini ya Utendaji Kazi wa Wizara na Taasisi zake ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA), Wakala wa Nishati Vijijini ( REA), Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja ( PBPA), Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania
(TGDC).

Viongozi wa Wizara walioshiriki Mkutano huo ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Umeme na Nishati Jadidifu, Dkt. Khatibu Kazungu, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mafuta na Gesi, Dkt. James Mataragio pamoja na Menejimenti ya Wizara.

# KATIBU MKUU NISHATI AIPONGEZA SWEDEN KUFADHILI MIRADI YA UMEME NCHINI

- Yakabidhi Mradi wa umeme wa Makambako-Songea
- Ufadhili wake Mradi wa Makambako- Songea wawezesha vijiji 120 kupata umeme
- Ni nchi ya kwanza kufadhili miradi ya umeme vijijini nchini




Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha.Felchesmi Mramba akizungumza na Waandishi wa Habari pamoja na wageni waalikwa jijini Dodoma wakati wa hafla ya kufunga rasmi Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea, uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden na Tanzania.

Balozi wa Sweden nchini atoa pongezi kwa TANESCO na REA usimamizi wa miradi ya umeme

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba ameipongeza Serikali ya Sweden kwa kuimarisha ushirikiano na Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya umeme ikiwa ni pamoja na mradi wa Makambako hadi Songea.

Pongezi hizo zimetolewa Februari 27, 2025 jijini Dodoma wakati wa hafla ya kufunga rasmi Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea, uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Mhandisi Mramba amesema kuwa mradi huo wa njia ya umeme kutoka Makambako hadi Songea umehusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 220 kwa urefu wa kilomita 245, ujenzi wa vituo vya umeme vya Madaba na Songea mjini, upanuzi wa kituo cha umeme cha Makambako pamoja na kusambaza umeme katika vijiji 120.

"Tunaipongeza Serikali ya Sweden kwa mchango mkubwa ambao wanatusaidia katika kufadhili miradi mbalimbali ya umeme ikiwemo kupeleka umeme vijijini hapa nchini." Amesema Mramba

Amesema kuwa, Serikali ya Sweden imetoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini iliyotekelezwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya za Urambo, Serengeti, Simanjiro na Ukerewe, pia Sweden ndio nchi ya kwanza kusaidia miradi ya umeme vijijini hapa nchini.




Balozi wa Sweden nchini Tanzania Mhe. Charlotta Ozaki Macias akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma wakati wa hafla ya kufunga rasmi Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea, uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mha.Gissima Nyamo-Hanga akizungumza jambo wakati wa hafla ya kufunga rasmi Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea uliofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Miradi mingine iliyofadhiliwa na Sweden ni mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mtera na Kidatu.

Ameongeza kuwa, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Sweden kwa sasa inaendeleza ukarabati wa kituo cha kuzalisha umeme cha Hale ambacho ni cha muda mrefu ambacho kitazalisha megawati 21 baada ya ukarabati kukamilika. Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mhe. Charlotta Ozaki Macias ameipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya umeme.

Amesema mradi wa Makambako hadi Songea uliotekelezwa kwa kipindi cha miaka 20 kukamilika kwake kutaendelea kunufaisha wananchi wengi katika upatikanaji wa huduma ya umeme hasa maeneo ya vijijini.

# WAKANDARASI WASIMAMIWE KUTEKELEZA MIRADI YA NISHATI KWA WAKATI - KAPINGA

- Aagiza wasimamiwe kwa karibu kumaliza miradi
- Awataka Watendaji TANESCO kuwa na mahusiano mazuri na wananch



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO, na wakuu wa taasisi za wizara kabla ya kushiriki ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan inayotarajiwa kuanza leo mkoani Tanga.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amewataka watendaji wa Sekta ya Nishati kuwajengea uwezo watoa huduma wanaotekeleza miradi mbalimbali ya sekta ya nishati nchini.

Hayo ameyasema Februari 23, 2025 na Kapinga wakati akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO, na wakuu wa taasisi za wizara kabla ya kushiriki ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan inayotarajiwa kuanza leo mkoani Tanga.

"Tunataka hii miradi ikamilike kwa wakati na kwa ubora mkubwa, wakandarasi wajengewe uwezo wa utendaji kazi ili kazi ionekane inafanyika,"Ameongeza Mhe. Kapinga.

Aidha, ameipongeza REA kwa kumaliza kufikisha umeme kwenye vijiji vyote nchini na kusisitiza miradi inayoendelea na ile inatakayoanza mwaka huu wa fedha itekelezwe kwa wakati.

"Ni muhimu sana kuwasimamia wakandarasi kwa nguvu kuanzia mwanzo tuwe nao makini ili miradi hii ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ikamilike kwa wakati, " Amesema Mhe. Kapinga

Katika hatua nyingine, Mhe. Kapinga amewataka watendaji wa taasisi za nishati kuwa na mahusiano mazuri na wananchi hususan wakati wa kupitisha miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Imarisheni mahusiano na wananchi mnapopitisha miradi yetu na kuwaeleza kuwa Serikali italipa fidia kwa wote miradi hiyo ilipopita," Amesema Mhe. Kapinga.

# AFRIKA TUNAPASWA KUTUMIA RASILIMALI TULIZONAZO KUZALISHA UMEME WA KUTOSHA - DKT. BITEKO

- Asema pamoja na dunia kuhamia kwenye nishati jadidifu, makaa ya mawe yatasaidia Afrika kuwa na umeme wa kutosha
- Aeleza mafanikio sekta ya nishati Tanzania katika Jukwaa la Mawaziri Wiki ya Nishati India
- Tanzania yapongezwa kwa miradi ya kikanda ya umeme




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko,( katikati) akizungumza wakati aliposhiriki katika mjadala wa Mawaziri wa Sekta ya Nishati kutoka India, Qatar, Uingereza na Tanzania wenye mada iliyosema Mpango Mpya wa Dunia wa Biashara ya Nishati ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa Wiki ya Nishati India.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa pamoja na dunia sasa kuweka mkazo ikiwemo ya kifedha kwenye uzalishaji umeme kwa kutumia nishati jadidifu kama vile jua, maji na upepo, nchi za Afrika zinapaswa kutumia vyanzo ilivyonavyo kama vile makaa ya mawe ili kuweza kuwa na umeme wa kutosha.

Dkt. Biteko amesema hayo Februari 11, 2025, New Delhi, India wakati akishiriki katika mjadala wa Mawaziri wa Sekta ya Nishati kutoka India, Qatar, Uingereza na Tanzania wenye mada iliyosema Mpango Mpya wa Dunia wa Biashara ya Nishati ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa Wiki ya Nishati India.

Dkt.Biteko ametolea mfano kuwa Tanzania ina madini ya makaa ya mawe ya kutosha pamoja na urani ambayo yanafaa kuzalisha umeme hata hivyo kumekuwa na changamoto ya kupata ufadhili wa kuyaendeleza kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa vile yanatajwa kusababisha uchafuzi wa mazingira akieleza kuwa makaa ya mawe yanaweza kutumika kuzalisha umeme kwa kutumia teknolojia ya kisasa yenye kuondoa sumu ya kaboni.

Amesema kuwa takribani watu milioni 600 barani Afrika hawajafikiwa na huduma ya umeme hivyo kwa kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ikiwemo makaa ya mawe itawezesha lengo la kufikishia umeme watu hao kwa haraka.

“ Afrika inachangia uchafuzi wa mazingira kwa kiasi kidogo kwa sababu ni bara maskini lakini inatajwa kuwa na mchango sawa na mataifa mengine, mabadiliko ya matumizi ya nishati hayakwepeki, nchi ziruhusiwe kuwa na uendelezaji endelevu wa rasilimali zake kwa ajili ya kuwa na usalama wa nishati.” amesisitiza Dkt. Biteko.

Ameongeza "Lazima tuangalie ukweli na hali halisi mfano Qatar au India hali yao ya upatikanaji umeme ni tofauti na Tanzania, hatutaweza kutumia njia ya aina moja kwa ajili ya kutatua changamoto za masuala ya umeme kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea ni lazima kutumia njia tofauti,"

Ameangazia lengo la Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi Afrika (Mission 300) uliofanyika nchini Tanzania hivi karibuni wa kufikisha nishati ya umeme kwa watu milioni 300 barani humo ifikapo mwaka 2030 na kusisitiza kuwa pia Afrika inahitaji fedha na miundombinu ya kusafirisha umeme pamoja na vyanzo mseto vya uzalishaji umeme ili kufikisha lengo la kuwapatia umeme wananchi wake kwa asilimia 100.

Pamoja na hayo, Dkt. Biteko amebainisha mafanikio ya sekta ya nishati nchini Tanzania na kusema kuwa kuna umeme wa kutosha huku ziada ikiwa ni megawati 750 na kwamba imejenga miundombinu ya kusafirisha na kuunganisha umeme na nchi jirani kama vile Kenya, Burundi na Rwanda ili kuwezesha biashara ya umeme.

Waziri anayeshughulikia masuala ya nishati kutoka Uingereza, Mhe. Ed Milliband ameipongeza Tanzania kwa mafanikio yake katika uzalishaji na usambazaji umeme kwa wananchi na hasa miradi ya umeme kwenda katika nchi jirani.

Kwa upande wake, Waziri wa Petroli na Gesi kutoka nchini India, Mhe. Hardeep Singh Puri amesema kuwa

Mkutano huo wa Nishati India unalenga kuwakutanisha pamoja viongozi wa sekta ya nishati, watunga sera na wavumbuzi kutoka maeneo mbalimbali duniani ili kujadili changamoto zilizopo katika sekta hiyo na kutafuta suluhushi kwa mustakabali endelevu wa upatikanaji wa nishati.

Aidha, utaangazia teknolojia za kisasa, mipango kabambe ya kupunguza uzalishaji kaboni na fursa za uwekezaji zinazoendana na malengo ya nishati kimataifa

# DKT. BITEKO ATEMBELEA UBALOZI WA TANZANIA NCHINI INDIA



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na Watanzania waishio India pamoja na watumishi wa Ubalozi wa Tanzania nchini India mara baada ya kumaliza ziara nchini humo zilioanza Februari 10 - 14, 2025 jijini New Delhi ( Februari 14, 2025)


Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametembelea Ubalozi wa Tanzania nchini India na kuzungumza na Watumishi katika ofisi hiyo.

Akizungumza katika Ofisi hizo jijini New Delhi, Dkt. Biteko alempongeza Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbega kwa mapokezi mazuri na kazi nzuri zinazofanywa na Ubalozi huo ikiwemo kutangaza fursa za uwekezaji.

" Nakushukuru kwa mapokezi mazuri mliyotupatia tangu tulipofika hapa kwa kweli yamerahisisha utekelezaji wa majukumu yetu, mnaipa heshima kubwa Serikali kwa namna ambavyo Ofisi hii inavyohudumia watu mbalimbali wenye uhitaji wanapokuja hapa ikiwemo watu wanaoonesha nia ya kuwekeza Tanzania au Watanzania wanaotaka kuwekeza hapa India." Amesema Dkt. Biteko

Amesema ushiriki wa Wizara ya Nishati katika Mkutano wa Wiki ya Nishati India umekuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo kuhamasisha ushiriki wa wawekezaji mbalimbali katika duru ya tano ya kunadi vitalu vya mafuta na gesi asilia.

Ameongeza kuwa " Kwa upande wa Wizara ya Nishati tutajitahidi watu wanapotoka India kuja Tanzania kama wawekezaji tuwape



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati waliokaa) akiwa kwenye picha ya pamoja na Uongozi wa wanafunzi wanaosoma nchini India ambao alikutana nao akiwa ziarani nchini humo Februari 14, 2025 jijini New Delhi. Wa pili kulia ni Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, Wa kwanza kulia ni Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Iddi Kassim na Wa Pili kushoto ni Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe.Anisa Mbega.


ushirikiano mzuri,"

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Iddi Kassim amesema Kamati hiyo imefarijika kwa kupata fursa ya kushiriki Wiki ya Nishati nchini India ambapo wamejifunza masuala mbalimbali na kupata uzoefu katika usimamizi wa sekta ya nishati hasa ikitambulika kuwa India imepiga hatua kubwa kwenye nishati.

Dkt. Biteko amemaliza ziara yake ya siku tano nchini humo ambapo anarejea nchini Februari 15, 2025.

Awali, Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbegai alimshukuru Dkt. Biteko kwa ziara ambayo amesema kuwa imewaheshimisha kama wenyeji wa Ujumbe wa Tanzania nchini India.

" Nitumie fursa hii kukupongeza kwa majukumu yako uliyotekeleza ukiwa hapa na tunakushukuru kwa heshima kubwa uliyotupatia." Amesema Mbega



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwa kwenye picha ya pamoja na Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbega mara baada ya kutembelea Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini India zilizopo New Delhi Februari 14, 2025 jijini New Delhi

Aidha, Mhe. Mbega ametaja baadhi ya majukumu ya Ofisi ya Ubalozi kuwa ni kuimarisha uhusiano baina ya nchi za uwakilishi, kulinda maslahi ya nchi na kuhakikisha fursa mbalimbali zinapatikana kama vile masoko, utalii na uwekezaji.

# SERIKALI, SEKTA BINAFSI KUIMARISHA HUDUMA ZA FEDHA NCHINI

- Dkt. Biteko afungua tawi la Exim Benki Kahama
- Exim yachangia vifaa vya matibabu vya shilingi milioni 25 Hospitali ya Wilaya Kaham




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua Tawi la Benki ya Exim Wilayani Kahama, Shinyanga Februari 25, 2025.

Uzinduzi wa tawi la Exim Bank Kahama ni uthibitisho wa ukuaji wa sekta ya benki, ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali na dhamira ya kukuza uchumi wa wananchi. Aidha, Serikali imekuwa ikihimiza taasisi za fedha kuipeperusha bendera ya Tanzania nje ya nchi kwa kufanya uwekezaji wa kimkakati.

Hayo yameelezwa Februari 25, 2025 Kahama mkoani Shinyanga na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko wakati akizindua tawi la Benki ya Exim.

" Kahama ni kitovu kikubwa cha shughuli za kiuchumi, hasa sekta ya madini ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa. Zaidi ya madini, mji huu pia ni maarufu katika sekta ya kilimo na biashara. Ni wazi kuwa ufanisi wa sekta hizi unategemea upatikanaji wa huduma za kifedha imara na zinazokidhi mahitaji ya wajasiriamali na wafanyabiashara," amesema Dkt. Biteko.

Ameendelea "Hivyo, kwa kufungua tawi hili, Exim Benki inatoa fursa ya kipekee kwa wakazi wa Kahama kupata huduma za kifedha zinazoendana na shughuli zao za kiuchumi. Na kunaleta manufaa makubwa kwa jamii ya hapa Kahama, kwa wateja wengine wa benki na benki yenyewe kwa ujumla,"

Dkt. Biteko ametaja manufaa hayo kuwa ni kuongezeka kwa fursa za uchumi kwa kuongeza ajira, kuongeza mapato ya benki na hivyo kutumia sehemu ya faida yake kuchangia maendeleo ya jamii ikiwemo kusaidia makundi maalum kadhaa yenye uhitaji yaani (Corporate Social Responsibility - CSR)

Aidha, manufaa mengine ni kuongezeka kwa mapato ya kodi Serikalini na kuongezeka kwa ushindani wa huduma za kibenki.

Pia, Dkt. Biteko ameipongeza benki hiyo kwa hatua kubwa na kwa jitihada zake za kuleta huduma za kifedha karibu zaidi na



wananchi pamoja na kuiwakilisha Tanzania katika nchi za Comoros, Uganda, Djibouti, pamoja na Ethiopia.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameipongeza Benki ya Exim kwa kuisaidia jamii kupitia Exim Cares " Nimefurahi kusikia kuwa kabla ya kuzindua wa tawi hili tayari mmechangia vifaa vya matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama vyenye gharama ya zaidi ya shilingi milioni 25. Mchango huo wa vifaa vya matibabu utasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Kahama. Hatua kama hizi zinaonesha mshikamano wa sekta binafsi na Serikali katika kuboresha ustawi wa wananchi."

Pia, amesema kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha huduma za kifedha na kuhakikisha kuwa zinapatikana kwa urahisi na kwa ufanisi kwa kila Mtanzania.

Vilevile, Dkt. Biteko ametoa wito kwa Benki hiyo kuwashika mkono na kuwakuza vyema wananchi wa kawaida na wa hali ya chini ambao wao watakuwa ni wateja muhimu. Aidha, uchumi wa wananchi hao wa kawaida hukuwa kwa kasi kutokana na shughuli zao za kiuchumi na hivyo kuisaidia pia benki kukua.

Benki hiyo ya Exim inatarajiwa kuwasaidia wananchi wa Kahama wanaohitaji huduma za kibenki ili kukua kiuchumi kwa kutoa huduma mbalimbali kama vile fursa za kufungua akaunti, kupata mikopo, na kufanikisha malipo mbalimbali kwa njia salama na rahisi zaidi.

" Niwatoe wasiwasi Benki ya Exim kuwa Kahama inafedha na inaendelea kukuwa kwa sababu ya uwepo wa bandari kavu na katika sekta ya madini mfano Kabanga nikeli na bidii ya watu wa hapa ya kufanya kazi. Hapa ni soko kubwa na muone fahari watu wa Kahama wanatajirika kupitia benki yenu," amemalizia Dkt. Biteko.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Anamringi Macha amesema kuwa ufunguzi wa tawi la benki hiyo ni kielelezo kuwa shughuli za uchumi ni nyingi na zitaendelea kuimarishwa.

Ameongeza kuwa Mkoa huo una matawi ya benki 11 ambayo yote pia yapo Kahama hivyo ni kiashiria kuwa Kahama ipo kibiashara na kuwa Mkoa huo uko tayari kushirikiana na benki hiyo.

Naye, Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja amesema kuwa Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kifedha na kuwa dira iliyopo imekuwa ikiwaongoza na ni mpango mkuu wa sekta ya fedha ulioandaliwa na Serikali umeweka mazingira wezeshi na moja ya manufaa yake ni kufunguliwa kwa tawi hilo la benki.

Akitaja idadi ya benki zilizopo nchini amesema kwa sasa kuna benki 44, matawi zaidi ya 1000 na wakala wa huduma za kibenki zaidi ya 100,000 na hivyo ukuaji wa benki umeongezeka.

" Wizara tunaipongeza kwa dhati Benki ya Exim kwa kufungua tawi Kahama na kusogeza huduma hizi karibu na wananchi," amesema Dkt. Mwamaja.

Pamoja na hayo, amesema kuwa kumekuwepo na changamoto ya watoa huduma wasio waaminifu na mikopo chechefu, hivyo Wizara kupitia Benki Kuu imeendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kutoa elimu ya masuala ya fedha mijini na vijijini ili wananchi waelewe na kutumia fursa za fedha zilizopo.



Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja akizungumza wakati wa uzinduzi wa Tawi la Exim Kahama, Shinyanga Februari 25, 2025.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Benki ya Exim Tawi la Kahama. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Anamringi Macha na Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Exim Jaffari Matundu.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu amesema kuwa uzinduzi huo unathibitisha dhamira ya benki hiyo ya kuleta suluhu ya masuala ya fedha na uwekezaji ambapo mwaka 1997 walizindua tawi la kwanza jijini Dar es salaam na kwa sasa taasisi hiyo ina wigo mpana wa kutoa huduma zake.

“ Benki yetu imekuwa ikishirikiana mwa karibu na watu wa Kahama kwa shughuli mbalimbali ambapo tumewajulisha wakazi kuhusu huduma zetu na kuwa mshirika wa kudumu wa fedha,” amesema Bw. Matundu.

Aidha, amesema benki hiyo si tu imesaidia katika sekta ya afya bali hata elimu, ubunifu na kuwezesha wajasiriamali wanawake.

“ Tutaongeza ushiriki wa kifedha kutoka kwa wafanyabiashara na wananchi wanaotafuta suluhu ya kifedha kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika shughuli zao,” amebainisha Bw. Matundu

# KUPITIA KONGAMANO LA PETROLI LA EAC TUNATAKA NISHATI YA PETROLI IWE INJINI YA MAENDELEO - DKT.MATARAGIO

- Tanzania kuchimba visima vya utafutaji Mafuta Eyasi Wembere
- CNG kufika hadi kwenye mikoa ambayo haijafikiwa na Bomba la Gesi



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.James Mataragio akizungumza katika Kipindi cha Jambo Tanzania kinachoendeshwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ikiwa ni muendelezo wa programu za kutoa elimu kwa umma kuhusu Kongamano na Maonesho ya 11 ya Petroli ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Machi 5-7 mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.James Mataragio amesema Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Afrika Mashariki ( EAPCE'25 ) ambayo yatafanyika Machi 5 hadi 7 mwaka huu jijini Dar es Salaam yanalenga kuhakikisha kuwa nishati ya petroli inakuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo kwenye Jumuiya ya Afrika.Mashariki.

Amesema hayo tarehe 26 Februari 2025 jijini Dar es Salaam katika Kipindi cha Jambo Tanzania kinachoendeshwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ikiwa ni muendelezo wa programu za kutoa elimu kwa umma kuhusu Kongamano na Maonesho ya 11 ya Petroli ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Machi 5-7 mwaka huu.

Amesema Tanzania ina rasilimali kubwa ya gesi ambayo iligunduliwa mwaka 1974 Songosongo iliyoanza kuzalishwa mwaka 2004 ambayo inatumika kwenye viwanda, magari, majumbani na kwa kiasi kikubwa inatumika kuzalisha umeme.

Ameeleza kuwa, hivi karibuni shughuli za utafutaji mafuta zimeanza kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Bonde la Eyasi Wembere ambapo Serikali inatarajiwa kuanza kuchimba visima vya utafutaji mafuta huku dalili zikionesha kuwa eneo hilo lina rasilimali husika.

Amesema kupitia EAPCE' 25 nchi zitabadilishana uzoefu katika masuala ya utafutaji wa mafuta huku Tanzania tayari ikiwa imeanza kubadilisha uzoefu na Uganda hasa ikizingatiwa kuwa nchi hiyo tayari imeshagundua rasilimali husika.

Kuhusu utekelezaji wa Nishati Safi ya Kupikia kupitia mradi wa kusambaza gesi majumbani unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) amesema kuwa, mradi huo ni endelevu na mikoa iliyo pembezoni mwa mkuza wa bomba la gesi kutoka Mtwara imeendelea kusambaziwa nishati hiyo.

Ameeleza kuwa, Serikali pia inatilia mkazo ujenzi wa vituo vya kujazia gesi kwenye magari (CNG) ambayo itasafirishwa kwenye mikoa ambayo bado haijafikiwa na bomba la gesi. Amesema ujenzi wa vituo hivyo unahusisha sekta binafsi.

Dkt.Mataragio ameeleza kuwa mwaka huu vitazinduliwa vituo 6 vya CNG ambapo mwezi ujao kitazinduliwa kituo kikubwa cha CNG katika eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam.

Kuhusu Mkutano wa EAPCE' 2025 amesema umekuja wakati muafaka kwani unaleta wadau wote wa nishati ya petroli kutoka Afrika Mashariki na nchi nyinginezo ambao utatumika pia kama sehemu ya kujadili upatikanaji wa nishati ya kutosha ili kufikia malengo ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Misheni 300 ambao uliazimia kufikisha umeme kwa waafrika milioni 300 ifikapo 2030 .

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji TPDC, Derrick Moshi amesema kuwa Mkutano wa EAPCE utajumuisha makundi mbalimbali ikiwemo wafanyabiashara na wawekezaji kwenye Sekta ya Mafuta, taasisi za kifedha, Wakandarasi wanaojihusisha na Sekta ya Mafuta, Watendaji kutoka Serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Watafiti.

Amesema Mkutano utafungua fursa nyingi katika Sekta ya Nishati pamoja na sekta nyinginezo.

Ameongeza kuwa Mkutano huo utatumika kunadi vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia kupitia Duru ya Tano ya kunadi vitalu hivyo.

# SERIKALI IMEIMARISHA USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UONGOZI NA SHUGHULI ZA KIUCHUMI-KAPINGA

- Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani atoa wito wa kushikamana



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga, akizungumza wakati alipokuwa akielezea nafasi ya mwanamke katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo nchini yatafanyika mkoani Arusha.

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema kuwa Serikali imeboresha mazingira ya wanawake nchini ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi, maendeleo ya Tanzania na kushika nafasi za uongozi.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo alipokuwa akielezea nafasi ya mwanamke katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo nchini yatafanyika mkoani Arusha.

"Kipekee namshukuru na kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani amekuwa dira ya kutuongoza na kuhakikisha wanawake wengi zaidi tunashiriki katika shughuli za maendeleo na hata katika nafasi za uongozi." Amesema Mhe. Kapinga

Amesema Rais Samia amekuwa kinara katika kuibua wanawake katika sekta mbalimbali za kiuchumi nchini.

Ameitaka jamii kuondokana na dhana kwamba mwanamke anapopewa nafasi ya uongozi anaweza kusahau majukumu yake mengine ya kijamii.

Aidha, Mhe. Kapinga ametoa wito kwa wanawake kupendana, kushikamana, kusaidiana na kutembea kifua mbele katika kuelekea Siku ya Wanawake Duniani.

# DKT. BITEKO AWASILI NCHINI INDIA KWA ZIARA YA KIKAZI

- Kushiriki Mikutano ya Kimataifa na Wiki ya Nishati ya India
- Mawaziri wa Nishati, Watunga Sera na Wavumbuzi wa teknolojia za Nishati kukutana


Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko Februari 11, 2025 amewasili nchini India kwa ajili ya kushiriki mikutano mbalimbali ya kimataifa ya nishati ambayo inaenda sambamba na Maadhimisho ya Tatu ya Wiki ya Nishati ya India mwaka 2025 (India 3rdAnnual Energy Week) kuanzia tarehe 11 hadi 14 Februari, 2025.

Katika Uwanja wa Kimataifa wa Indira Gandhi, jijini New Delhi, Dkt.Biteko amepokelewa na Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. AnisaMbega na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mafuta na Gesi India,Sandeep Jain.


Wiki ya Nishati India itakutanisha Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Sekta ya Nishati kutoka maeneo mbalimbali duniani, Watonga sera na wavumbuzi wa teknolojia mbalimbali za kisasa za nishati kwa lengo la kuja na mustakabali endelevu wa upatikanaji nishati.

Aidha, Wiki hiyo itahusisha pia maonesho ya teknolojia mbalimbali za matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia

Katika ziara hiyo, Dkt.Biteko ameambatana na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na baadhi ya Watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakiongozwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (kulia) akiwa na Balozi wa Tanzania nchini India, Mhe. Anisa Mbega mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Kimataifa wa Indira Gandhi, jijini New Delhi nchini India kwa ajili ya kuhudhuria mikutano mbalimbali ya kimataifa kuhusu nishati.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko akikaribishwa nchini India na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mafuta na Gesi India, Sandeep Jain mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Indira Gandhi katika Jiji la New Delhi kwa ajili ya kushiriki mikutano mbalimbali ya kimataifa kuhusu nishati.

# DKT.KAZUNGU AFANYA MAZUNGUMZO NA WAJUMBE KUTOKA SHIRIKA LA MAENDELEO LA SAUDIA

- Yakabidhi Mradi wa umeme wa Makambako-Songea
- Ufadhili wake Mradi wa Makambako- Songea wawezesha vijiji 120 kupata umeme
- Ni nchi ya kwanza kufadhili miradi ya umeme vijijini nchini




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Dkt. Khatibu Kazungu amekutana na ujumbe kutoka Shirika la Maendeleo la Saudia (Saud Fund for International Development (SFD) na kufanya mazungumzo kuhusu utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kutoka Benaco wilayani Ngara hadi Kyaka wilayani Misenyi pamoja na kituo cha kupooza umeme cha Benaco mkoani Kagera.

Kikao kazi hicho kimefanyika jijini Dodoma, Februari 19, 2025.

Dkt. Kazungu ameishukuru SFD kwa ufadhili wake katika miradi mbalimbali nchini ikiwemo miradi ya Nishati na kuahidi kuwa Wizara itaendelea kushirikiana nao katika kufanikisha miradi hiyo ukiwemo mradi wa Benaco - Kyaka ambao unafadhiliwa kwa ushirikiano baina ya SFD, OPEC na ADFD. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai mwaka huu.

Ujumbe wa SFD uliongozwa na Ahmed Al Misfer ambaye ni Msimamizi wa Miradi katika shirika hilo

# KAMATI YA WATAALAM NISHATI SAFI YA KUPIKIA WAJADILI UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Yakabidhi Mradi wa umeme wa Makambako-Songea
- Ufadhili wake Mradi wa Makambako- Songea wawezesha vijiji 120 kupata umeme
- Ni nchi ya kwanza kufadhili miradi ya umeme vijijini nchini



Kamati ya wataalam iliyoundwa na Maafisa Waandamizi kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Nishati safi ya Kupikia kitaifa imekutana kujadili utekelezaji wa mkakati huo wenye lengo la kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Kikao kazi hicho kimefanyika katika Ofisi za Wakala wa Nishati Vijijini ( REA ) jijini Dodoma Februari 5,2025 ambapo Maafisa Waandamizi hao wamepitia taarifa mbalimbali za utekelezaji na kutoa mapendekezo yaliyolenga kuboresha nyaraka hizo kabla ya kuziwasilisha katika Kamati ya Makatibu Wakuu.

Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia ni Ajenda ya Kitaifa inayohakikisha wananchi wanaondokana na matumizi ya nishati isiyo safi ikiwemo kuni na mkaa.

Mwenyekiti wa Kikao kazi hicho, Bw. Omari Ilyas ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Uratibu wa Shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu amesisitiza utekelezaji wa mkakati huo usiwe na kikwazo hivyo bajeti za utekelezaji wa mkakati wa nishati safi ya kupikia zinapaswa kutengwa.

"Wizara na taasisi zote kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanatakiwa kutekeleza mkakati huu kwa kiwango kikubwa na bajeti zitengwe ili utekelezaji wa mkakati uwe na tija." Amesema Ilyas

Kamati hiyo pia ilipokea wasilisho na kufanya maboresho ya rasimu ya mwongozo wa uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia iliyoainisha majukumu ya wadau wote ili kufanikisha uratibu husika kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati.